TANGAZO LA SERIKALI NA. 86 tarehe 17/2/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI
(SURA YA 355)

---

# AMRI

---

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1))*

---

## AMRI YA KUPANGA ENEO LA SEGERA-MICHUNGWANI YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itaitwa Amri ya Kupanga eneo la Segera-Michungwani ya Mwaka 2023.

Kutangaza Eneo la Upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Kuandaa na Kuhifadhi Mipango ya Jumla na ya Kina.

3. Mipango ya Jumla na ya Kina ya eneo lililoainishwa kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo: -

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba GY412 yenye majira - nukta 439610MS, 9406789KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa umbali wa kilomita 8.67 katika uelekeo wa 89°.58'.27'' hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba NP1 yenye majira - nukta 448343MS, 9406798KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi kwa umbali wa kilomita 2.3 katika uelekeo wa 76° 50' 48''hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P1 yenye majira - nukta 450559MS, 9407309KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa umbali wa kilomita 0.98 katika uelekeo wa 11° 21' 33''hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P2 yenye majira – nukta 450743MS, 9408266KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi kwa umbali wa kilomita 3 katika uelekeo wa 341° 56' 38'' hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VTB109 yenye majira - nukta 449782MS, 9411136KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi kwa umbali wa kilomita 3.7 katika uelekeo wa 26° 15' 30''hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba TV190 yenye majira - nukta 451127MS, 9414626KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa kufuata uelekeo wa mto Pangani hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VTB270 yenye majira - nukta 449893MS, 9420493KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki kwa umbali wa kilomita 2.7 katika uelekeo wa 77° 43' 21'' hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VTB92 yenye majira - nukta 447216MS, 9419902KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki kwa umbali wa kilomita 7.5 katika uelekeo wa 56° 36' 41''hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba TV194 yenye majira – nukta 440952MS, 9415831KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa umbali wa kilomita 5 katika uelekeo wa 29° 46' 38''hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba TV198 yenye majira – nukta 438931MS, 9411765KZ; hadi ulipoanzia".

Dodoma
6 February, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*